# Mtawanyiko wa Nomino za Ki-Bena za Asili moja Kisemantiki katika Ngeli za Msingi wa Kimofolojia

*F.J. Mwendamseke*

*Ikisiri*

Kutokana na vigezo fulani vya kiisimu, nomino huainishwa katika makundi kadhaa ambayo hujulikana kama ngeli za nomino (Kihore na wenzie, 2008). Mgawanyiko huu wa nomino katika ngeli unaweza kukitwa katika msingi wa kimofolojia (maumbo) au Kisemanti (kimaana). Hivyo, katika kupanga makundi ya nomino katika ngeli kisemantiki (maana) husababisha mtawanyiko wa nomino za msingi wa kimofolojia katika ngeli mbalimbali. Hii inatokana na changamoto zilizopo katika misingi ya kinadharia ya uainishaji ngeli katika lugha za Kibantu. Lakini mtawanyiko huu huweza kutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine kutegemeana na upekee wa lugha hiyo. Ingawa lugha za Kibantu zina mfumo wa ngeli, kuna utofauti fulani unaojitokeza miongoni mwa lugha hizo (Maho, 1999). Lengo la makala haya ni kuchunguza mtawanyiko wa nomino zenye asili moja kisemantiki katika ngeli za msingi wa kimofolojia katika Ki-Bena. Imebainika kuwa mtawanyiko wa nomino katika Ki-Bena upo katika nomino za viungo vya mwili, matunda na wanyama. Mtawanyiko wa nomino haupo kabisa katika nomino zinazotaja majina ya binadamu. Hii inatofautiana sana na lugha nyingine kama vile Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Ki-Bena ni miongoni mwa lugha za Kibantu na huzungumzwa maeneo ya nyanda za juu Kusini-Magharibi mwa Tanzania katika mkoa wa Njombe. Guthrie (1967/1971) aliainisha lugha hii katika ukanda wa G60 unaoitwa Bena-Kinga. Kutokana na uwepo wa lahaja mbalimbali katika Ki-Bena, uchunguzi huu unahusu lahaja ya Ki-Maswamu inayozungumzwa Kusini-Magharibi mwa mkoa wa Njombe. Wesana - Chomi (2001:44) amefasili maana ya ngeli kuwa ni "kundi" au "aina". Hivyo katika taaluma ya isimu mgawanyo wa makundi mbalimbali ya nomino ambao umekitwa katika misingi ya uwiano wa kisarufi hujulikana kama ngeli. Neno ngeli linatokana na neno la kihaya, *engeli,* lenye maana ya *aina* (Mgullu, 1999).

Uainishaji wa ngeli za nomino ni utaratibu unaotumika katika kuzipanga nomino za lugha katika makundi mbalimbali kwa kufuata mfanano wa viambishi ngeli (Ashton, 1944 na Katamba, 2003). Utaratibu huu wanaozungumzia Ashton (1944) na Katamba (2003) unafuata mkabala au vigezo vya Kimofolojia. Massamba na wenzie (2001) wamefasili *mofolojia* kuwa ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchambuzi wa mfumo wa maneno katika lugha, yaani muundo wa maneno (maumbo). Kwa mfano, katika Kiswahili umoja na wingi wa nomino nyingi huelezwa kwa viambishi dhahiri, kwa mfano *ki-tabu* (umoja) na *vi-tabu* (wingi). Hivyo, kwa kutumia kigezo cha kimofolojia, Khamisi na Kiango (2002) wanaeleza kuwa ngeli ya nomino inaweza kutambuliwa kutokana na umbo la nomino linalohusika kama umbo

lenyewe linaruhusu viambishi au la.

Ngeli pia huainishwa kwa kutumia kigezo cha kisemantiki, ambacho hujikita katika maana. Kwa hiyo, kigezo cha kisemantiki katika uainishaji ngeli za nomino ni utaratibu wa kupanga nomino katika makundi kwa kuzingatia maana ya ujumla inayofungamanisha kundi zima la nomino zinazohusika (Massamba, 1995). Kwa misingi hiyo, katika kila ngeli ya nomino kuna maana fulani zinazojitokeza ambazo hutumika katika kuziweka nomino fulani katika ngeli moja. Kwa mfano, katika lugha za Kibantu Ngeli ya 1-2, inajumuisha nomino zinazohusu binadamu, na nomino hisivu nyinginezo (Mutaka na Tamanji, 2000). Uainishaji ngeli kisemantiki husababisha mtawanyiko wa nomino zenye asili moja kisemantiki zilizoundwa kwa msingi wa kimofolojia kama msingi mkuu. Kwa mfano, katika Kiswahili, zipo nomino ambazo zinawiana kisemantiki, na hivyo, nomino hizo zinaweza kuwekwa katika ngeli moja. Hata hivyo, nomino hizo zikiainishwa kimofolojia zinapangwa katika ngeli tofauti. Kwa mfano, nomino *kiongozi* katika Kiswahili ambayo imepangwa kwenye ngeli ya {ki-/vi-}, imeorodheshwa kwenye ngeli hiyo kutokana na uainishaji wa kimofolojia. Kwa upande mwingine, nomino *mtoto* ipo katika ngeli ya {m-/wa-}. Japokuwa kisemantiki, nomino hizo zilitakiwa ziwe katika ngeli moja inayohusu watu na viumbe hisivu, uainishaji wa kimofolojia unazitawanya nomino hizo.

Kwa misingi hiyo kuna tatizo la kupanga katika ngeli tofauti za nomino za asili moja kisemantiki kutokana na kutumia kigezo cha kimofolojia. Changamoto inajitokeza katika kazi za wanaisimu mbalimbali kama vile Ashton (1944), Zawawi (1974) Polomé (1976) na Gibbe (1983). Hawa wameainisha ngeli katika lugha ya Kiswahili. Kihore na wenzie (2008) wanaeleza kuwa nomino nyingi zenye matatizo kama hayo ni zile za majina ya watu, ndege na samaki. Wanafafanua kama ifuatavyo:

> *"nomino zinazohusu majina ya watu, wanyama, ndege, samaki, na viumbe wa aina yake huweza kuwa na viambishi vya nomino za ngeli nyingine* (uk.125). "

Katika kufafanua hoja hii walitumia nomino *kipofu anaimba* na *vipofu wanaimba*. Katika mfano huu, msingi wa uainishaji ngeli kimofolojia, nomino *kipofu* huweka katika ngeli ya 7/8 {ki-/vi-}. Kutokana na hali hii mwandishi wa makala haya aliona kwamba kuna haja ya kuchunguza hali ikoje katika Ki-Bena.

**2.0 Mtawanyiko wa Nomino za Ki-Bena zenye Asili Moja Kisemantiki**

Katika kufanikisha lengo la makala haya nomino za Ki- Bena ziliainishwa

katika makundi mbalimbali kwa kufuata mkabala wa kisemantiki ili kuona mtawanyiko wa nomino ukoje. Ufuatao ni uainishaji huo:

Jedwali 1: Ngeli za Ki-Bena- Mkabala wa Kisemantiki

| Na.Ng | KNg | Al | Mfano | Tafsiri | Maana |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mu- | m-mw-Ø | umunu, umdimi | 'mtu', 'mvulana' | Vitu vyenye uhai, (majina ya binadamu tu) |
| 2. | va- | | avanu, avadimi | 'watu', 'wavulana' | |
| 3. | mu- | m- | umubuyu,umlomo, | 'mbuyu','mdomo' | Matunda, wanyama, baadhi ya viungo vya mwili na vitu vya kijozi |
| 4. | mi- | | imibuyu, imilomo, | 'mibuyu', 'midomo' | |
| 5. | li- | | iligulu , ilisebetu | 'mguu','koleo' | Mimea, miti, matunda na baadhi viungo vya mwili vya viumbe hai |
| 6. | ma- | | amagulu , amasebetu | 'miguu','makoleo' | |
| 7. | hi- | sh- | ihinu , ishala | 'kitu' , 'kidole' | Viungo vidogovidogo vya mwili, wanyama wadogo wadogo na vitu visivyo na uhai |
| 8. | fi- | fy- | ifinu , ifyala | 'vitu','vidole' | |
| 9. | Ø - | | ing'onde , ikaye | 'kondoo', 'nyumba' | Majina ya mkopo, aina za wanyama, ndege, samaki na baadhi ya viungo vya mwili |
| 10. | Ø - | Ø - | ing'onde , ikaye | 'kondoo' , 'nyumba' | |
| 11. | lu- | | ulusahulwa,ulukandzi | 'nyuzi','ngazi' | Vitu vyenye umbo refu, jembamba au bapa |
| 12. | ha- | | ahana, ahadembwe | 'katoto','katembo' | Udogoshaji |
| 13. | tu- | tw- | utwana, 'utudembwe' | 'tutoto' 'tutembo' | |
| 14. | wu- | | uwudesi, uwubaya | 'uongo' , 'ubaya' | Nomino dhahania (zisizoonekana wala kushika. Pia nomino zisizohesabika |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 15. | hu- | | uhukina, uhutova | 'kucheza' ,'kupiga' | Nomino zote zinazotokana na vitenzi. (hutokana na mchakato wa unominishaji kwa kutumia {ku-} |
| 16. | pa- | | apala, apamutwe | 'pale', 'juu ya kichwa' | Zinahusu mahali |
| 17. | hu- | | uhula, uhumutwe | 'kule' ,'katika kichwa' | |
| 18. | mu- | | umula, umumutwe | 'mule','ndani ya kichwa' | |

**Ufunguo:**
Na. Ng = Namba ya Ngeli
KNg = Kiambishi Ngeli
Al = Alomofu

Kutokana na uainishaji huu wa ngeli kisemantiki imedhihirika kuwa zipo nomino fulani zinazowiana kisemantiki. Nomino hizo zingaliweza kupangwa katika ngeli moja, lakini kwa kutumia kigezo cha kimofolojia zimepangwa katika ngeli tofauti.

Katika Ki-Bena, nomino zinazotaja majina ya binadamu ikiwa ni pamoja na zile zinazotaja walemavu, zimeundwa kimofolojia kwa viambishi vya umoja na wingi vinavyopatikana katika ngeli ya 1/2 Viambishi hivyo ni {mu-, m-, mw-, Ø / na va-}, (Mwendamseke, 2011). Hali hii imezifanya nomino zote zinazotaja majina ya binadamu kupangwa katika ngeli ya 1/2. Baadhi ya nomino hizo zimeorodheshwa katika mfano *(1)* hapa chini:

(1) Nomino katika Ngeli ya 1/2 *{mu-, m-, mw-, Ø /va-}*

| Na | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kibena** | **Kiswahili** | **Kibena** | **Kiswahili** |
| (a) | udado | baba | avadado | baba |
| (b) | umbufu | kipofu | avabufu | kipofu |
| (c) | udereva | dereva | avadereva | madereva |
| (d) | umunu | mtu | avanu | watu |
| (e) | umwana | mtoto | avana | watoto |
| (f) | Umdibafu | kiziwi | uvadibafu | kiziwi |

Mifano hiyo hapo juu inaonesha kuwa katika Ki-Bena, nomino za binadamu ikiwa ni pamoja na zile zinazotaja walemavu, ndugu na jamaa kama vile dada, baba, kilema, mtu, zote zinabeba viambishi ngeli vya umoja na wingi vilivyopo katika ngeli ya 1/2. Hali hii ni tofauti katika lugha nyingine kama vile Kiswahili, ambapo maneno kama hayo huambikwa viambishi ngeli tofauti na

kuainishwa katika ngeli tofauti. Kwa mfano, nomino *kipofu* katika ngeli ya 7/8 zenye viambishi ngeli {ki-/vi-}, *baba* katika ngeli ya 9/10 zenye viambishi ngeli {N-/N-}, *dereva* katika ngeli ya 5/6 zenye viambishi ngeli {Ø-/ma-} na mtu katika ngeli ya 1/2 zenye viambishi ngeli {m-/wa-}.

Kutokana na nomino zote zinazotaja majina ya binadamu kuambikwa viambishi ngeli vilivyo sawa katika Ki-Bena, hairuhusu kabisa nomino zinazohusu binadamu kutawanyika katika ngeli nyingine. Hivyo, kigezo cha kisemantiki katika Ki-Bena kinatudhihirishia kuwa binadamu amepewa hadhi ya juu kuliko viumbe wengine. Hali hii inadhihirishwa na ukweli kwamba, nomino zinazohusu majina ya binadamu hazichanganywi kabisa na nomino za makundi mengine.

Hata hivyo, katika Ki-Bena, kuna aina nyingine za nomino ambazo zimetawanywa kimofolojia katika ngeli tofautitofauti ingawa kisemantiki zilitakiwa ziwe zimepangwa pamoja. Nomino zilizoathiriwa zaidi ni zile zinazotaja viungo vya mwili, matunda na wanyama kama zinavyoonesha hapo chini:

## 2.1 Mtawanyiko wa Nomino za Viungo vya Mwili katika Ngeli Mbalimbali

Nomino zinazohusu viungo vya mwili zinapatikana katika ngeli ya 3/4 zenye viambishi ngeli {m-/mi-}, ngeli ya 5/6 zenye viambishi ngeli {li-/ ma-}, ngeli ya 9/10 zenye viambishi ngeli kapa {Ø- /Ø-} na ngeli ya 7/8 zenye viambishi ngeli {hi-/fi-}. Nomino hizo katika Ki-Bena zinaoneshwa katika mfano *(2 i-iv)* hapa chini:

(2) ( i) *Nomino katika Ngeli ya 3/4 {m-/mi-}*

| **Na** | **Umoja** | | **Wingi** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kibena** | **Kiswahili** | **Kibena** | **Kiswahili** |
| (a) | umlomo | mdomo | imilomo | midomo |
| (b) | umtwe | kichwa | imitwe | vichwa |
| (c) | umgongo | mgongo | imigongo | migongo |

*( ii) Nomino katika Ngeli ya 5/6 {li-/ma-}*

| **Na** | **Umoja** | | **Wingi** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kibena** | **Kiswahili** | **Kibena** | **Kiswahili** |
| (a) | ilipaja | paja | amapaja | mapaja |
| (b) | iliwokho | mkono | amawokho | mikono |
| (c) | ilisihizda | sikio | amasihidza | masikio |

( iii) *Nomino katika Ngeli ya 9/10 {Ø-/Ø-}*

| Na | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kibena** | **Kiswahili** | **Kibena** | **Kiswahili** |
| (a) | ikwapa | kwapa | ikwapa | kwapa |
| (b) | isingo | shingo | isingo | shingo |
| (c) | imula | pua | imula | pua |

( iv) *Nomino katika Ngeli ya 7/8 {hi-/fi-}*

| Na | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kibena** | **Kiswahili** | **Kibena** | **Kiswahili** |
| (a) | i**hi**gudi | kiuno | ifigudi | viuno |
| (b) | i**hi**fuva | kifua | ififuva | vifua |
| (c) | ihisigino | kisigino | ifisigino | visigino |

Katika data hii, imedhihirika kwamba nomino zihusuzo viungo vya mwili zipo katika ngeli hizo tofautitofauti. Ukiangalia katika mfano (2i) inadhihirisha bado kuna tofauti fulani baina ya Kibena na Kiswahili. Kwa mfano, nomino *kichwa* katika Ki-Bena (umtwe) ipo katika ngeli ya 3/4 lakini katika lugha ya Kiswahili ipo ngeli ya 7/8.

## 2.2 Mtawanyiko wa Nomino za Matunda katika Ngeli Mbalimbali

Maho (1999) anaeleza kuwa katika uainishaji wa kisemantiki wa Mame-Bantu, nomino zinazohusu matunda zinatakiwa ziwe katika ngeli ya 5/6 tu. Lakini katika Ki-Bena nomino hizi huweza kuainishwa katika ngeli ya 3/4 zenye viambishi ngeli [m-/mi-], na ngeli ya 5/6 zenye viambishi ngeli *{li-/ma-}*. Nomino hizo katika ngeli ya 3/4 na ngeli ya 5/6 katika Ki-Bena zinaoneshwa katika Mfano *(3i-ii)* hapa chini:

**(3) ( i)** *Nomino katika Ngeli ya 3/4 {m-/mi-}*

| Na | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kibena** | **Kiswahili** | **Kibena** | **Kiswahili** |
| (a) | umtong'oni | zabibu | imitong'oni | zabibu |
| (b) | umfelegedzi | 'felegezi' | imifelegedzi | 'felegezi' |
| (c) | umkusu | 'kusu' | imikusu | 'kusu' |

**( ii)** *Nomino katika Ngeli ya 5/6 {li-/ma-}*

| Na | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kibena** | **Kiswahili** | **Kibena** | **Kiswahili** |
| (a) | ilinanasi | nanasi | amananasi | mananasi |
| (b) | ilidzungwa | chungwa | amadzungwa | machungwa |
| (c) | ilipera | pera | amapera | mapera |

Mifano iliyotolewa hapo juu inaonesha kuwa katika Kibena nomino za matunda ya asili ya Kibena zinapatikana katika ngeli ya 3/4, wakati nomino za

matunda zilizokopwa kutoka lugha nyingine kama vile Kiswahili, zipo katika ngeli ya 5/6.

## 2.3 Mtawanyiko wa Nomino za Wanyama katika Ngeli Mbalimbali

Nomino hizi huainishwa katika Ki-Bena kwenye ngeli ya 9/10 ambayo haina viambishi ngeli dhahiri {Ø-/Ø-} na ngeli ya 5/6 zenye viambishi ngeli {li-/ma-}. Nomino hizo katika ngeli za Ki-Bena zinaoneshwa katika mfano wa *{4i-ii}* hapa chini:

(4) (i) *Nomino katika Ngeli ya 5/6 {li-/ma-}*

| Na | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kibena** | **Kiswahili** | **Kibena** | **Kiswahili** |
| (a) | ilififi | fisi | amafifi | fisi |
| (b) | ilikoho | simba | amakoho | simba |
| (c) | ilidembwe | tembo | amadembwe | tembo |
| (d) | ilibwa | mbwa | amabwa | mbwa |

(ii) *Nomino katika Ngeli ya 9/10 {Ø-/Ø-}*

| Na | Umoja | | Wingi | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kibena** | **Kiswahili** | **Kibena** | **Kiswahili** |
| (a) | ing'onde | kondoo | ing'onde | kondoo |
| (b) | isenga | ng'ombe | isenga | ng'ombe |
| (c) | imene | mbuzi | imene | mbuzi |

Katika mtawanyiko huu wa nomino hizi zinazohusu aina za wanyama kuna upekee fulani unajitokeza katika Ki-Bena tofauti na baadhi ya lugha nyingine za Kibantu kama vile Kiswahili (Kiango, 1992) na Ki-Matumbi (Odden, 1996). Kwa mtazamo wa wanaisimu hao, katika Kiswahili na Ki-Matumbi nomino za wanyama hupatikana katika ngeli ya 9/10 tu. Lakini katika Ki-Bena nomino hizo zimetawanyika katika ngeli mbalimbali ambapo nomino nyingi zinazohusu wanyama wa porini zinapatikana katika ngeli ya 5/6, wakati nomino za wanyama wengi wa kufugwa, zinapatikana katika ngeli ya 9/10. Nomino ya mbwa ndiyo kighairi pekee, ambayo hupatikana katika ngeli ya 5/6 badala ya ngeli ya 9/10.

## 3.0 Hitimisho

Makala haya yamechunguzwa kwa ufupi mtawanyiko wa nomino za Ki-Bena kisemantiki zilizoundwa kwa msingi mmoja wa kimofolojia. Imedhihirika kuwa nomino zinazohusu binadamu hazitawanyiki kabisa katika ngeli nyingine bali zipo katika ngeli ya 1/2 tu. Matokeo haya yanatofautiana na hali ilivyo kwenye baadhi ya lugha za Kibantu kama vile Kiswahili (Taz. § 2.0). Hata hivyo, mtawanyiko huu umejidhihirisha katika nomino za makundi mengine ya nomino zisizo binadamu. Nomino hizo ni zile zinazohusu matunda, wanyama

na viungo vya mwili wa binadamu. Tatizo la mtawanyiko huu linatokana na ukweli kwamba msingi mkuu wa uainishaji ngeli unaotumika ni wa kimofolojia. Hii inatokana na misingi ya kinadharia ambayo hutupatia changamoto katika uainishaji ngeli za nomino katika lugha za Kibantu. Kwa hiyo, ili kuepuka tatizo hili ni vema uainishaji ngeli kwa msingi wa kisemantiki ufanyike peke yake bila kuchanganya na msingi wa kimofolojia ili kupunguza matatizo yanayojitokeza katika uainishaji ngeli. Aidha, kuna haja ya kufanya uchunguzi zaidi kuhusiana na misingi ya uainishaji ngeli za nomino katika lugha mbalimbali za Kibantu ili kuweza kubaini kwa uwazi kabisa utata unaojitokeza katika mtawanyiko wa nomino hizo katika ngeli mbalimbali hasa kutokana na athari ya kisemantiki katika ngeli za nomino. Hii itasaidia kuelewa uelekeo wa jumla na nini kifanyike ili kupunguza au kuondoa utata huo.

Ashton, E.O. (1944). *Swahili Grammar, (including intonation).* London: Longman Group Ltd.

Gibbe, A.G. (1983). "Uchambuzi wa Nomino za Ngeli ya Kwanza Katika Kiswahili", Katika TUKI, *Lugha ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI, uk. 244 – 256.

Kahigi, K. K. (2005). "The Sisumbwa Noun: It's Classes and Derivation", katika *Occasional Paper in Linguistics.* Dar es Salaam: LOT. Uk. 117-154

Katamba, F. (2003). "Bantu Nominal Mophology" katika Nurse na Philippson, *The Bantu Languages*. Routledge: London.

Khamisi, M.A. na J. G. Kiango (2002). *Uchanganuzi wa Sarufi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria.

Kiango, J.G.. (1992). *Swahili Dictionary Design.* Columbia University: Tasnifu ya PhD (Haijachapishwa).

Kihore, Y.M, D.P.B. Massamba na Y.P. Msanjila, (2008). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA).* Dar es Salaam, TUKI.

Maho, J. (1999). *A Comparative Study of Bantu Noun Classes.*Goteborg Universty, Tasnifu ya PhD (Haijachapishwa).

Massamba, D.P.B. (1995). "The Classification of Ci-Ruri Nouns", katika *Journal of Asian and African Studies,* Na.48-49. ILCAA, Tokyo University of Foreign Studies.

Massamba, D. P. B. Kihore, Y.M na Hokororo J.I. (2001). *Sarufi Miumbo ya Kiswahili* (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, S.R. (1999). *Mtaala wa Isimu.* Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Mutaka, N. na Tamanji, P.N. (2000). *Introduction to African Linguistics*. Muenchen: Lincom Handbooks in Linguistics.

Mwendamseke, F. (2011). *Uainishaji wa Ngeli za Nomino katika Lugha ya Ki-Bena.* Tasnifu ya M.A. Haijachapishwa (Kiswahili) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Odden, D. (1996). *The Phonological and Morphology of Kimatumbi.* New York: Oxford University Press.

Polomé, E.C. (1976). *Swahili Language Handbook.* Washington D.C, Center for Applied Linguistics.

Wesana – Chomi E. (2001). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Sebha, Libya: African Studies Research Centre.

Zawawi, K. (1974). *Loan Words and their Effect on the Classification of the Swahili Nominals: A Mophonological Treatment.* Tasnifu ya PhD Haijachapishwa Chuo Kikuu cha Columbia.